

HALMASHAURI YA MJI KOROGWE



08/12/2017

TANGAZO LA ZABUNI – MARUDIO II

ZABUNI NA. LGA/126/NC/2017/2018/02

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Korogwe anawatangazia wananchi waishio Korogwe wenye sifa na wafanya biashara wote, zabuni kwa ajili ya kuwapata mawakala wa kukusanya mapato mbalimbali ya Halmashauri pamoja na kuwapata wapangaji wa majengo mbalimbali ya Halmashauri. Wananchi/Kampuni/Kikundi/Ushirika na wafanyabiashara wote wenye sifa zinazohitajika mnakaribishwa kuleta maombi yenu.

Zabuni hizi zimegawanyika katika makundi mbalimbali kama ifuatavyo:-

1. Kundi la I - Kupangisha vyumba vya Booking Office stendi mpya ya Kilole Vyumba 8
2. Kundi la II – Kupangisha viosk (Vibanda) 12 katika viosk (55) stendi mpya ya Kilole- Mtu binafsi asiye na kampuni au kikundi anaruhusiwa kuomba.
3. Kundi la III- Kupangisha viosk (Vibanda) 17 katika viosk (49) stendi mpya ya Kilole- Mtu binafsi asiye na kampuni au kikundi anaruhusiwa kuomba.
4. Kundi la IV- Kupangisha vyumba viwili(2) jengo la Park Hotel- Mtu binafsi asiye na kampuni au kikundi anaruhusiwa kuomba.
5. Kundi la V –Kupangisha vyumba vinne (4) jengo la Hekuse - Mtu Mtu binafsi asiye na kampuni au kikundi anaruhusiwa kuomba.
6. Kundi la VI - Kupangisha KTC Kantini- asiye na kampuni au kikundi anaruhusiwa kuomba
7. Kundi la VII – Kumpata mzabuni wa kutoa huduma ya **Supermarket** stendi mpya ya Kilole.
8. Kundi la VIII – Kumpata mzabuni wa kukusanya ushuru wa mazao mchanganyiko na misitu
9. Kundi la IX – Ukusanyaji wa ushuru choo cha soko la sabasaba

MASHARTI KWA WAOMBAJI:

1. Mwombaji lazima awe na leseni hai kwa biashara husika, mwombaji aonyeshe utambulisho wa mlipa kodi (TIN), usajili wa kampuni, kama amesajiliwa kwenye VAT basi aonyeshe usajili wa VAT, Uhalali wa kisheria kusaini nyaraka (power of attorney).
2. Mwombaji lazima ataje kiwango atakacholipwa na Halmashauri kutoka kwenye makusanyo.(%) kwa mwezi. Makusanyo yote yaingizwe kwenye akaunti ya Halmashauri.
3. Waombaji wa kupanga majengo ya Halmashauri wakati wa kuomba inabidi kwenye maombi yao waambatanishe picha zao za passport size
4. Maombi yote yatalipiwa kiasi cha Tshs 50,000/= fedha ambazo hazirudishwi.Unapoleta maombi kumbuka kuweka stakabadhi uliyolipia ada ya uzabuni.Maombi kwa njia ya fax/email hayatakubaliwa. Isipokuwa Kantini Ada ya waombaji itakuwa Tsh.20,000/= fedha hairejeshwi
5. Waombaji wa viosk/vibanda vya biashara watalipa kodi ya miezi sita kabla ya kusaini mkataba. Waombaji wengine watalipa dhamana ya mwezi mmoja ya kiwango cha mkataba kabla ya kusaini mkataba
6. Muombaji wa viosk (vibanda) stend mpya lazima awe mkazi wa Korogwe
7. **Vikundi vya kinamama na vijana vitakavyojitokeza kuomba zabuni yeyote vitapewa kipaumbele.**
8. Maombi yote yafungwe kwenye bahasha kwa lakiri na juu ya bahasha andika zabuni unayoomba. Maombi yote yatumwe kwa:-

**KATIBU WA BODI YA ZABUNI
HALMASHAURI YA MJI
S.L.P 615 - KOROGWE.**

2. Mwisho wa kupokea maombi ni 21/12/2017 saa 5.00 asubuh, maombi yoyote yatakayoletwa baada ya saa 5.00 hayatapokelewa na ufunguzi utafanyika siku hiyo hiyo saa 5.10 asubuhi katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri. Halmashauri hailazimiki kukubali au kukataa zabuni yoyote ile na uamuzi wa Halmashauri ndio wa mwisho.Tangazo hili limetolewa na :-

**JUMANNE K. SHAURI
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA MJI - KOROGWE**